**Taarifa kwa vyombo vya habari**

**Rais Kenyatta awa Mwenyekiti wa Umoja wa Marais wa Afrika wa Kupambana na Malaria**

*Kutangaza dira yake ya mapambano dhidi ya malaria barani Afrika*

**Addis Ababa, Februari 10, 2020** – Rais wa Kenya, Mheshimiwa Uhuru Kenyatta, ameteuliwa kuwa mwenyekiti wa Umoja wa Marais wa Afrika wanaopambana na malaria ujulikanao kama African Leaders Malaria Alliance (ALMA). ALMA ni Umoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali walioungana pamoja katika kuongeza juhudi za kutoa elimu na kutafuta fedha ili kusaidia kupambana na kuutokomeza ugonjwa wa malaria ndani ya bara la Afrika. Rais Kenyatta anakuwa mwenyekiti wa saba wa umoja huo na atashikilia kiti hicho kwa muhula mmoja wa miaka miwili kuanzia Februari 2020 mpaka Februari 2022. Anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Mfalme Mswati III wa Eswatini.

Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta, alisema: "Ninayo heshima kubwa kupata nafasi kuwa mwenyekiti wa ALMA. Tayari kuna mafanikio makubwa kwenye mapambano dhidi ya malaria, japo tumerudi nyuma kidogo katika miaka ya hivi karibuni. Tunapoingia kwenye muongo wa kumaliza kabisa ugonjwa huu, ninayo nia ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunayaendeleza mafanikio tuliyokwisha yapata ili kutokomeza kabisa malaria. Jambo kubwa kabisa kwenye Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063: ni kuona kwamba tunakuwa na Afrika yenye watu wenye afya njema, wachapa kazi watakaosaidia kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya jamii."

Wakati wa muhula wake, Mfalme Mswati III alitoa mchango mkubwa kwenye uanzishwaji wa kampeni ya kutokomeza malaria iliyoitwa *Bila Malaria inawezekana-inaanza na mimi* (*Zero Malaria Starts with Me)* ambayo mpaka sasa iko katika mataifa 13. Mfame Mswati III pia alianzisha chapisho la kila mwaka la maendeleo ya vita dhidi ya malaria lililoitwa *Africa Malaria Progress Report* pamoja na wakfu maalum wa kuunga mkono juhudi za kumaliza kabisa malaria huko Eswatini.

Mfalme Mswati III alisema: "Tulifurahi kufanya kazi hii tulipokuwa na uenyekiti wa ALMA na tutaendelea na juhudi za kutokomeza malaria kwa Waafrika wote. Tayari tunaona nchi nyingine zinavyoanzisha wakfu zao maalum kwa ajili ya kutokomeza malaria na matarajio yetu ni kuona jambo hili linaenea kote barani Afrika."

Ugonjwa wa malaria unabaki kuwa changamoto kubwa inayolikabili bara la Afrika. Kiasi cha 93% ya wagonjwa wote wa malaria duniani wanapatikana Afrika huku 94% ya vifo vyote ulimwenguni vinavyotokana na malaria navyo vikitajwa kutokea barani humo. Kuna haja ya kuchukua hatua za haraka hasa katika mataifa 10 yaliyoko ndani ya Umoja wa Afrika ambayo yanachangia 67% ya wagonjwa na 62% ya vifo ulimwenguni kote.

Kamishina wa Masuala ya Jamii wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Mheshimiwa Amira El-Fadil, alisema: "Kutokomeza ugonjwa wa malaria barani Afrika ni kipaumbele namba moja kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa kutokomeza UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria na tumejidhatiti kuhakikisha tunafanikiwa. Ninamkaribisha Mheshimiwa Rais Kenyatta kama Mwenyekiti wa ALMA na tutampa ushirikiano wa kutosha ili kutokomeza janga hili.

Dr. Abdourahmane Diallo, Mtendaji Mkuu wa ushirikiano wa RBM wa kutokomeza Malaria, alimkaribisha mwenyekiti mpya wa ALMA akisema: “Uongozi toka kwa Wakuu wa Nchi za Kiafrika ni muhimu sana katika kufikia lengo la kuuondoa kabisa ugonjwa huu barani Afrika. ALMA ni jukwaa mahsusi na muhimu na mshirika mzuri wa Ushirikiano wa RBM katika kutokomeza malaria. Matarajio yetu ni kuendelea na ushirikiano huu na kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais Kenyatta katika kutokomeza malaria sio tu nchini Kenya lakini kote barani Afrika.

Tangu mwaka 2009, ALMA imekuwa na jukumu kubwa la kuchochea uwajibikaji katika vita dhidi ya malaria ndani ya bara la Afrika. Kupitia mikakati maalum ya uwajibikaji, na mfumo wa ufuatiliaji uchukuaji wa hatua, Wakuu wa Nchi na Serikali wanaweza kufuatilia maendeleo na kuchochea uwajibikaji kwa ajili ya kudhibiti na kutokomeza kabisa ugonjwa huo. ALMA pia inaunga mkono mataifa kwenye uanzishwaji wa Mabaraza ya Kutokomeza Malaria na Wakfu, na hata juhudi mbalimbali zinazosaidia kuongoza uwajibikaji wa viongozi na wanasiasa katika mapambano ya kutokomeza malaria.

******Mwisho*****

**Kuhusu ALMA**

ALMA ambayo ilianzishwa mwaka 2009, ni Umoja wa Viongozi wa Afrika wanaopambana kutokomeza malaria. Unawajumuisha Wakuu wa Nchi na Serikali wanaofanya kazi nje ya mipaka na kanda zao kutokomeza kabisa malaria ifikapo mwaka 2030. Nchi zote za Umoja wa Afrika (AU) ni wanachama wa ALMA. Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea: www.alma2030.org

**Iwapo una maswali, tafadhali wasiliana na:**

Tawanda Chisango
Email: tchisango@alma2030.org
Simu: +263 71 906 6647

Eugene Nganga (Nairobi)
Email: eugene.nganga@portland-communications.com
Simu: +254 703 516 173

**Tufuate kwenye:**
Facebook: www.facebook.com/ALMA-African-Leaders-Malaria-Alliance-356455541093491
Twitter: https://twitter.com/alma_2030
LinkedIn: https://www.linkedin.com/company/african-leaders-malaria-alliance-alma-/
Flickr: www.flickr.com/photos/103141785@N06